JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

***Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa:***

**Tel:** +255 262 965732 (Direct line)
+255 659 566703
***e-mail***: ded@sikongedc.go.tz
***Tovuti***: sikongedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge
4 Mtaa wa Bomani
S.L.P 70
**45382 - SIKONGE TABORA**

**13/07/2023**

# TANGAZO

# LA

# KUTOA HUDUMA YA UKUSANYAJI TAKA NGUMU KATIKA SENTA ZA BIASHARA NA MAKAZI KATA YA SIKONGE NA MISHENI

## LGA/121/2023/2024/NC/05

1. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inapenda kuwatangazia wananchi wote wenye Vikundi au Makampuni yenye nia na uwezo wa kutoa huduma ya Usafi katika Ofisi za Halmashauri na maeneo mbalimbali yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Kazi hii ni kuanzia tarehe Agosti, 2023 hadi tarehe 30Juni, 2024.

2. Unakaribishwa kuleta Kotesheni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya II.

3. **Vitabu vya Kotesheni vinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa bei ya Tsh. 30,000/= ambayo haitarudishwa (non – refundable). kwa Vikundi au Kampuni itakayomba kazi hii**

4. Kotesheni zote zitumwe zikiwa zimejazwa nakala halisi (**ORIGINAL MOJA**) na nakala (**COPY MBILI**) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa;

**"KOTESHENI NA. LGA/121/2023 – 2024 /NC/05" KUTOA HUDUMA YA UKUSANYAJI TAKA NGUMU KATIKA SENTA ZA BIASHARA NA MAKAZI KATA YA SIKONGE NA MISHENI**

5. Maombi yote yapelekwe (yatumwe) kwa ***Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, S.L.P 70, SIKONGE.***

6. Kikundi au Kampuni iwe na Leseni halali ya Biashara na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake

7. Kikundi au Kampuni ionyeshe utambulisho kwamba inalipa Kodi (TIN Number) na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake

8. Kikundi au Kampuni iwe imesajiliwa na Msajili wa Makampuni au Vikundi na kivuli cha usajili kiambatanishwe kwenye maombi yake

9. **Kikundi au Kampuni ionyeshe kiasi cha fedha kwa asilimia (%) kitakachoilipa/ itakayoilipa Halmashauri kwa kila Mwezi.**

10. Mwombaji atafanya kazi ya kuzoa taka katika sehemu za kukusanyia taka (Vizimba)

11. Mwombaji atafanya kazi ya kusafirisha taka na kuzihifadhi

12. Mwombaji atafanya kazi ya kusafisha Mitaro kandokando ya barabara zote

13. Mwombaji atafanya kazi ya kukusanya tozo na ushuru wa huduma ya kukusanya taka kwa niaba ya Halmashauri kwa kutumia POS

14. Mwombaji anatakiwa afanye utafiti kwenye maeneo husika kabla ya kuwasilisha maombi ya zabuni anayaoomba.

15. Kikundi au Kampuni yenye Uzoefu itapewa kipaumbele kwa kuzingatia na vigezo vingine.

16. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni ***siku ya Jumatano tarehe 26.07.2023 saa 5:00 Asubuhi.*** Kotesheni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya waombaji au wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

17. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

Seleman Pandawe
Mkurugenzi Mtendaji (W)
**SIKONGE**

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE